TANGAZO LA SERIKALI NA 528 La tarehe 21/9/2018

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA

SURA. 287

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153)

SHERIA NDOGO ZA (KUANZISHWA KWA JUMUIYA ZA WATUMIAJI MAJI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kuanzishwa kwa Jumuiya za Watumiaji Maji) za Halmashauri ya Wilaya ya Newala za Mwaka, 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Newala.

Tafsiri

3. Katika sheria ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi ni pamoja na Afisa Mtendaji wa Kata au Kijiji;

"Chanzo cha Maji" maana yake ni kisima kilichoboreshwa

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya Newala.

"Halmashauri ya kijiji" maana yake ni Halmashauri ya kijiji ambacho chanzo cha maji kipo.

"Kijiji" maana yake ni Kijiji ambacho kimeanzishwa chini ya kifungu cha 22 cha Sheria Serikali za mitaa (mamlaka ya wilaya) sura ya 287.

Jumuiya ya Watumiaji Maji" maana yake ni muungano wa watu unaomiliki huduma ya maji na unaoundwa na watu binafsi au kaya zinazochota maji kwenye chanzo cha maji na ambao wamejiunga kwa hiari kuanzisha na kuendeleza huduma ya maji na usafi wa mazingira katika Kijiji au Kitongoji na ambacho kimesajiliwa kisheria na Halmashauri ya Wilaya. Taasisi na Jumuiya zinazotambulika kisheria zinaweza pia kuunda Jumuiya cha watumiaji maji ili kutambulika chini ya masharti haya.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Newala;

"Regista Maalum" maana yake ni daftari maalum lenye kuonyesha kumbukumbu za watumiaji maji wa jumuiya inayolindwa na masharti ya Sheria Ndogo hizi

Jumuiya ya Watumiaji Maji

4. Kutakuwa na Jumuiya za Watumiaji maji ambayo itasajiliwa na Halmashauri na kupewa Cheti kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(1) Jumuiya ya Watumiaji maji itapewa Cheti cha Umiliki wa eneo la chanzo cha maji lenye mzingo wa mita 60 na itatunza mazingira ya chanzo hicho katika hali ya usafi na kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha ulinzi na usalama wa mazingira hayo.

(2) Jumuiya kitakuwa na mkataba wa makubaliano juu ya umiliki, uendeshaji, matengenezo, usalama na kulinda afya na usafi wa mazingira ya chanzo cha maji na kujali makundi ya watu masikini katika Jamii.

Wajibu wa Jumuiya

5. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi wajibu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji utakuwa:-

(a) kulinda miundombinu na vyanzo vya maji.
(b) kusimamia upatikanaji wa uhakika wa huduma ya maji.
(c) kutoa elimu juu ya utumiaji kwa watumiaji maji.
(d) kusimamia maendeleo endelevu ya huduma ya maji.
(e) kuanzisha na kutunza rejista ya watumia maji.
(f) kusimamia mapato ya Jumuiya ya Watumia maji.
(g) kufanya ukarabati wa mradi.
(h) kuwasilisha Halmashauri taarifa ya mapato na matumizi ya kila mwezi

Wajibu kwa Halmashauri

6. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi wajibu kwa Halmashauri:-

(a) kusajili na kusimamia jumuiya ya watumia maji.
(b) kutambua na kuidhinisha vyanzo vya maji.
(c) kufatilia mara kwa mara utendaji kazi wa jumuiya.
(d) kuwezesha jumuiya kwa kutoa mafunzo.
(e) kutoa ushauri wa kitaalam kuhusiana na mradi wa maji.

Wajibu kwa watumiaji maji

Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi wajibu kwa Watumiaji Maji utakuwa:-

(a) kulipia huduma ya maji kwa kiwango kitakachokubaliwa.
(b) kutunza, Kulinda na kutumia vizuri miundombinu ya maji.
(c) kutoa taarifa ya uharibifu wa miundombinu wa huduma ya maji.

Wajibu wa Halmashauri ya Kijiji

7. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi wajibu kwa Halmashauri ya kijiji utakuwa ni kutoa ushauri; kuhamasisha; kuunga mkono; na kulinda Jumuiya za watumiaji maji zilizopo katika eneo la kijiji.

Mali za Jumuiya

8. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Jumuiya itakuwa na uwezo wa kumiliki mali.

(2) Hakuna mtu yeyote mwenye haki ya kuingilia mali za Jumuiya kwa namna yeyote ile.

(3) Hakuna mtu yeyote atakayedai kuwa mmiliki binafsi wa chanzo cha maji isipokuwa wanachama wa Jumuiya ya watumiaji maji.

Uwezo wa kukagua

9. (1)Afisa Mwidhiniwa, anaweza kwa wakati unaofaa, kuingia kwenye chanzo cha maji kwa lengo la kukagua na kuhakikisha kuwa Jumuiya ya Watumiaji maji inaendesha shughuli zake kwa kufuata taratibu za nchi.

(2) Afisa huyo atakuwa na uwezo wa kuchukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kushtaki mahakamani mtu au watu waliovunja masharti Sheria Ndogo hizi

Makosa

10. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo taasisi au mtu yeyote:-

(1) atatupa vitu vichafu, au kumwaga maji machafu, au taka nyingine au kuruhusu maji machafu kutapakaa au kutiririka kwenye chanzo cha maji.

(2) atajenga choo cha shimo au kuchimba shimo la taka au kulima ndani ya mita sitini kutoka kwenye chanzo cha maji.

(3) atasababisha vurugu au usumbufu kwa kuwasumbua watumiaji maji kwenye chanzo cha maji au mtu mwenye haki ya kuchota maji.

(4) atakataa kulipia huduma ya maji

(6) atafanya uvamizi, kuharibu au kuhujumu chanzo au miundombinu ya maji

Adhabu

11 Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) na isiyozidi shilingi laki tatu (Tsh.300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Tangazo la Serikali Na. 528(Linaendelea.)

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Newala uliofanyika mnamo Tarehe 24 Mwezi wa 04 Mwaka 2018 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

MUSSA M. CHIMAE
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya
Newala

L.S

RASHID CHITWANGA. NDEMBO,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya
Newala

NAKUBALI,

Dodoma,
27Agost 2018

SELEMANI S.JAFO (MB)
Waziri wa Nchi-or Tamisemi